**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2023**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**SHULE YA SEKONDARI ISMANI**

**Namba za Simu…………………..**

**Mkuu wa Shule- 0717364860/0753825060**

**Makamu Mkuu wa Shule-0752161569**

**Matron/Patron……………………**

**Shule ya Sekondari ISMANI**

**S.L.P. 378**

**Tarehe .12/06/2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI ISMANI HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA, MKOA IRINGA MWAKA 2023**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya **HGL, HKL, HGK, HGE na EGM**

Shule ya Sekondari Ismani ipo umbali wa Kilometa 42. kaskazini mashariki mwa mji wa Iringa katika Halmashauri ya **Wilaya ya Iringa.**Usafiri wa basi kutoka mjini unapatikana stendi ya mabasi ya **mkoa wa Iringa** Nauli ni Shilingi 2500/= hadi 3000/= kupitia barabara kuu ya kwenda Dodoma, na kama utatokea Dodoma kuelekea Iringa shuka katika kijiji cha Lwang'a-Ismani Tarafani.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **14/08/2023** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **13/08/2023**. Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31/08/2023**.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni sketi 2 nyekundu mshono wa rinda box yenye marinda isiyobana mwili na iwe ndefu kuishia kwenye enka za miguu (kitambaa kizito)
ii. Mashati meupe mawili ya mikono mirefu.
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.
iv. Sare ya Michezo (**T-shirt za blue 2 za Taifa stars na raba nyeusi moja).**
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;(jozi mbili na kuendelea)
vi. Soksi ndefu nyeupe jozi mbili na kuendelea.
vii. Sweta rangi ya blue **(shingo V**)
viii. Track suit rangi ya dark blue.
ix. Shamba dress (Gauni rangi ya dark-blue-mshono wa solo)
x. Skafu (ifanane na kitambaa cha sketi)
xi. T-shirt ya shule (inapatikana jirani na shuleni kwa Tsh 10,000)

**NB. Kwa wale wenye matatizo ya kiafya mfano kifua au pumu waje na puruneki nyeupe**.

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari (*counterbook kuanzia kumi*);

ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;(moja kwa kila muhula) Godoro futi 2 inchi 2 na nusu
iii. Mafaili mawili (Spring file za plastic). Kwa ajili ya kuwekea kumbukumbu muhimu za mwanafunzi.
iv. Scientific Calculator;
v. Brash ngumu moja yenye mpini mrefu kwa ajili ya usafi.
vi. Mashuka Jozi 2(rangi ya pinki na blue), blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1.
vii. Nguo za ndani za kutosha;
viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
ix. Ndoo 2 (moja lita Kumi na nyingine lita ishirini) zenye mifuniko;
x. Kwanja 1, jembe 1, na mifagio 2 ya chelewa.
xi. Begi la daftari.
xii. Toilet paper.
xiii. Mahitaji mengine ya kutosha ya mtoto wa kike.
xiv. Tochi moja ya betri au ya solar itakayotumika kukiwa na tatizo la umeme.
xv. Kamusi ya kingereza kwa wanaosoma tahasusi za lugha.
xvi. Sabuni za kutosha za kufulia na kuogea.
xvii. Matokeo ya mtihani wa Taifa wa kidato cha nne (**Result slip**

## 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa uendeshaji shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | Jumla | 80,000/= |

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.
xii. Mwanafunzi haruhusiwi kusuka nywele.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ………………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule –CHRISTOPHER B. MWASOMOLA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule -0717364860/0753825060.**
- **Makamu Mkuu wa Shule -0752161569.**
- **Mwandamizi Taaluma -0753757480.**
- **Mwandamizi Malezi -0767065968.**

**OFISI YA RAIS- TAMISEMI**

SHULE YA SEKONDARI ISMANI

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA KIDATO CHA TANO.**

(Sehemu ya kwanza ya fomu hii ijazwe na Mwanafunzi na sehemu ya pili ijazwe na Mzazi au Mlezi)

**SEHEMU YA KWANZA**

(Sehemu hii ijazwe na Mwanafunzi mwenyewe)

**picha**

Mimi ……………………………….. (Mwanafunzi) kwa hiari yangu nakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na kidato cha Tano katika Shule ya Sekondari Ismani. Aidha naahidi kutoshiriki/kutoanzisha migomo, fujo, kufuata sheria na kufanya makosa ya jinai.

Jina la Mwanafunzi …………………………………………………

Sahihi ya Mwanafunzi ………………………….

Tarehe …./…../20….

**SEHEMU YA PILI**

(Sehemu hii ijazwe na Mzazi/Mlezi)

Mimi ……………………………………………….. Mzazi/Mlezi wa ……………………………………………………………………………………………..
Nakubali nafasi aliyopewa mtoto wangu na kwamba muda WOTE awapo shuleni atalazimika kuwa mtii kwa Walimu, Wazazi, Viongozi na Jamii kwa ujumla. Atalazimika kufuata sheria zote za shule. Naahidi kuwa mwanangu atazifuata taratibu zote za shule hadi atakapo maliza shule.

Jina la Mzazi/ Mlezi ……………………………………………….

Sahihi ………………………………….

Tarehe …/…/20….

**OFISI YA RAIS- TAMISEMI**

**SHULE YA SEKONDARI ISMANI**

**FOMU YA KUKIRI KUKUBALI SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO YA SHULE**

**HABARI ZA MZAZI/ MLEZI**

(Fomu hii ijazwe na Mzazi /Mlezi)

Jina kamili la baba………………………………………………………………

Uraia ………………………………………………

Kazi yake …………………………………………………..

Jina kamili la mama ……………………………………………

Uraia …………………………………………..

Kazi yake ………………………………………..

(Jina kamili la mlezi (iwapo haishi na wazazi wake) ……………………………

Kazi na anuani ya Mlezi ……………………………………………

Mtoto anaishi na Baba tu, Mama tu, Wazazi wote au Mlezi ( kata yasiyohusika).

Dini ya Mzazi/Mlezi…………………………………………………

Dhehebu …………………………………………………

Anuani kamili ya sehemu ambako mtoto atakuwa anakwenda wakati wa

likizo……………………………………………………………………

Mimi ……………………………………………………… Mzazi/Mlezi wa ………………………. taarifa hiyo hapo juu ni sahihi. Naahidi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha kwamba mtoto wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi, na mwenye bidii.

……………………………………… ………………………………

Tarehe Saini ya Mzazi/Mlezi

MEDICAL EXAMINATION FORM

(**<u>To be completed by medical officer in respect of all new students</u>**)

Full name

…………………………………………………………………………………………..

Age ………………

1. Blood count ( red and white) …………………………………………………………
2. Urine examination
   ………………………………………………………………………………….
3. Stool examination
   …………………………………………………………………………………
4. Syphilis
   …………………………………………………………………………………………….
5. T.B Test
   ……………………………………………………………………………………………
6. Ear test
   …………………………………………………………………………………………….
7. Eye test
   ……………………………………………………………………………………………
8. Spleen
   ……………………………………………………………………………………………..
9. Pregnancy test
   ………………………………………………………………………………………
10. Abdomen
    ……………………………………………………………………………………………
11. Additional information or any other Physical, Mental, Hereditary of infectious diseases
    ……………………………………………………………………………………………
    ……………………………………………………………………………………………
    ………………

Treatment after examination

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

………………………..

**MEDICAL CERTIFICATE**

I certificate that the above concerned has been examined and found fit into pursue for further education.

Signature ……………………………
Designation ………………………..
Station ………………………………….

(Official stamp)
Date …./…./20…

**NB**: fomu hii ijazwe na Mganga katika Hospitali inayotambulika na serikali.

Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.

**VITABU PENDEKEZWA.**

**KISWAHILI**

1. Saluhaya C.M(2016): Nadharia Ya Lugha Kidato Cha Tano, Sita Na Elimu Ya Juu(toleo la pili. Ahmadiyya printers, Ya dare s sallam Tanzania
2. Saluhaya C.M (2012): Nadharia Ya Tahakiki Fasihi Ya Kidato Cha Tano Na Sita.
3. KILANGI . E. L (2019) NADHARIA YA FASIHI,KIDATO CHA 5 na 6
4. KILANGI .E.L (2019) TAHAKIKI KIDATO CHA 5 na 6
5. KILANGI .E.L (2019) NADHARIA YA LUGHA,KIDATO CHA 5 na 6

**HISTORY**

1.Salehe Yasini(2016):Essentials In Advanced Level History Paper2, Ahmadiyya printing press.
2. Shibitali c.k(2017): contemporary historical events , advanced level history 1, 3rd ED
3.Mwl. Bakari Madaya (2018): History paper one Lesson notes for Advanced Certificate of Secondary education. Based on the current Tanzania syllabus(2010)

GEOGRAPHY

1.David Waugh (2009): An integrated approach, 1010printing international ltd china.
2.Richard white (1984): African in focus, a physical human and economic geography.
3.C.R. Kothari (2008): Research methodology, new age International (p) limited publishers.
4.TIE (2016) GEOGRAPHY FOR SECONDARY SCHOOLS –FORM FIVE

ECONOMICS

1.C.M. Ambilikile ( ):Economics for Advanced and Professional Studies
2.Zist kamili( ): Economics for High Schools and Commercial Schools
3.N.S. SALEEMI(): Modern Economics.

**ENGLISH LANGUAGE**

**1.** LINGUISTIC CONCEPTS FOR ADV. LEVEL ENGLISH LG ONE BY JULTON SANGA (2017)

2. A RECOMMENDED ENGLISH LITERATURE HAND BOOK FOR A-LEVEL STUDENTS BY PASCHAL SALAWI 2014, 2015

3. ANALYTICAL ANALYSIS OF ADVANCED LITERATURE ENGLISH LANGUAGE FORM 5 & 6 BY MGONJA M. E (2019) First Edition.

4. ADVANCED LEVEL ENGLISH A PRACTICAL APROACH BY NICHOLAUS ASHELI (2014) Third edition

**MATHEMATICS**

1.SEPTINE I. SILLEM (2005): ADVANCED MATHEMATICS, 1ST ED, FORM FIVE
2.SEPTINE I. SILLEM (2015): ADVANCED MATHEMATICS. 1ST ED, FORM SIX

**BASIC APPLIED MATHEMATICS**

**3. TANZANIA INSTITUTE OF EDUCATION (2019):** Basic Applied Mathematics for Advanced Level Secondary Schools Student's Book**. Form Five and Six.**

**GENERAL STUDIES**

4. Mbalase. R, Richard( ): General Studies For Advanced Level Certificate Form Six And Form Five.